

- Kutoa huduma yenye kiwango na kudumisha kiwango husika
- Kufahamu wateja wako na kuwaridhisha
- Kufuata miongozo na kanuni za biashara husika
- Kufahamu mazingira yanayozunguka shughuli zako
- Kufahamu mahitaji ya bidhaa yako
- Kufahamu nguvu ya kiuchumi ya wateja wako.

## Utunzaji wa Kumbukumbu za Biashara

Ni muhimu kuwa na mfumo mzuri wa utunzaji wa kumbukumbu mbalimbali, ili kumwezesha mjasiriamali kufuatilia gharama za uzalishaji na uendeshaji, kupata habari za masoko na wateja wa bidhaa zake.

- Weka kumbukumbu ya kinachoingia na kutoka
- Weka kumbukumbu ya gharama za uzalishaji na uendeshaji
- Weka kumbukumbu na aina ya bidhaa na wateja wako.

*Imetayarishwa na Maabara ya Kitaifa ya Samaki chini ya Mpango wa TASP II kwa ufadhili wa mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya ya Ulaya (EDF)*

Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana na:

**AFISA MFAWIDHI WA KANDA  
NA MSIMAMIZI WA MRADI (TASP II)**  
KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI  
NA VIWANGO KANDA YA ZIWA VICTORIA  
S.L.P. 1213 MWANZA


**SIMU**

+255 28 2550864  
+255 754/784 437234

**Barua Pepe:** [nfqcl\\_mz@yahoo.co.uk](mailto:nfqcl_mz@yahoo.co.uk)

**Tovuti:** [www.nfqcl.go.tz](http://www.nfqcl.go.tz)

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI  
KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA  
SAMAKI NA VIWANGO



**Mbinu Bora  
na Endelevu za  
Ujasiriamali**



TRADE AND AGRICULTURE  
SUPPORT PROGRAMME II (TASP II)



# Mbinu Bora na Endelevu za Ujasiriamali

## Utangulizi

Ujasiriamali ni uwezo wa kubaini na utayari wa kuanzisha shughuli ya kiuchumi bila kujali hatari za kibiashara zinazoweza kujitokeza.

## Fursa za Ujasiriamali katika Uvuvi

- Kuna eneo kubwa la Uvuvi ambalo kila mmoja wetu anaweza kushiriki kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.
- Serikali kupitia sekta ya uvuvi imeweka mazingira rafiki ya

kuruhusu uwekezaji na kufanya biashara ya uvuvi na mazao yake.

- Kujihusisha na biashara nyingine zinazotoa huduma kwa shughuli za uvuvi.

## Faida ya Ujasiriamali katika Uvuvi

- Unakupa ajira na unaongeza kipato
- Unapanua wigo wa mahusiano ya kiuchumi na kijamii
- Unaongeza ajira kwa jamii

- Unapunguza uhalifu
- Kuchangia uhakika wa chakula.

## Mbinu za kuibua na kusimamia miradi

- Kuwa na wazo la kibiashara
- Kutathmini mahitaji (malighafi, bidhaa au huduma) ya mradi katika mazingira yaliyopo
- Kuandaa mpango wa biashara
- Kutafuta mtaji.

## Mbinu za kupata mitaji

- Kuunda vikundi vya ushirika wa uzalishaji
- Kuunda vikundi vya ushirika wa kuweka na kukopa
- Kuwasiliana na wadau wa maendeleo (k.m. asasi za serikali na zisizo za kiserikali, taasisi za fedha, n.k.)
- Kukusanya kidogo kidogo kutoka kwenye rasilimali binafsi.

## Aina na mbinu ya kupata na kushikilia masoko

- Uadilifu na uaminifu katika shughuli